



HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI



YAH: - TANGAZO LA MAOMBI YA MIKOPO YA VIKUNDI TAREHE 8/6/2022.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi anawatangazia Wananchi wote kutuma maombi ya Mikopo ya vikundi vya Wanawake, Vijana na watu wenye Ulemavu kwa robo ya nne ya mwaka 2022, Mikopo hiyo inatokana na 10% ya fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri.

- Wanawake 4%
- Vijana 4%
- Watu wenye ulemavu 2%

SIFA NA VIGezo MUHIMU VYA KUWEZA KUPATA MIKOPO HIYO:-


- Kikundi lazima kiwe kimesajiliwa (usajili mpya)
- Kikundi lazima kiwe na Akaunti Benki iliyo hai
- Kiwe na mradi au kinatarajia kuanzisha mradi
- Kisiwe na Mkopo/deni kutoka Taasisi nyingine ya Fedha
- Kikundi kisiwe na mwanachama mwenye ajira rasmi.
- Kiwe na Wadhamini wasiopungua watatu, wenye dhamana zisizo hamishika.

UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI YA MIKOPO:-

- Fomu za maombi zinapatikana ofisi za Mtendaji wa Kata/Ofisi za Halmashauri ya Wilaya.
- Kikundi kinapaswa kujaza nakala tatu (3) za fomu ya maombi.
- Fomu ya maombi ya mkopo iambatane na barua ya maombi iliyopitishwa na Afisa Mtendaji wa Kijiji pamoja na Muhtasari wa kikundi, ulioambatana na mahudhurio.
- Fomu zote zote za maombi ziwasilishwe ofisi ya Kata kwa Afisa Mtendaji wa Kata/ Afisa Maendeleo ya Jamii wa Kata husika kwa ajili ya Kuhakikiwa na kuwasilishwa kwa Mkurugenzi Mtendaji (W), S.L.P 20 Misungwi.

MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI NI TAREHE 30 /06/2022

Tangazo hili limetolewa na:


Benson P. Mihayo

**KAIMU: MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MISUNGWI.**



Jiandae kuhesabiwa tarehe 23, Agosti, 2022

**DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
MISUNGWI DISTRICT COUNCIL**